2 Yohana

Salamu

1 Mzee:
Kwa bibi mteule na watoto wake, niwapendao
katika kweli, wala si mimi tu, bali na wale wote
waijuayo kweli:
2 kwa sababu ya ile kweli ikaayo ndani yetu na
ambayo itaendelea kukaa nasi milele:
3 Neema, rehema na amani itokayo kwa
Mungu Baba na kwa Yesu Kristo, Mwanawe
Baba, itakuwa pamoja nasi katika kweli na
upendo.

Kweli Na Upendo

4 Imenipa furaha kuu kuona baadhi ya watoto
wako wanaenenda katika kweli, kama vile Baba
alivyotuagiza.
5 Sasa, bibi mpendwa, si kwamba
ninakuandikia amri mpya, bali ile tuliyokuwa
nayo tangu mwanzo. Tupendane kila mmoja na
mwenzake.
6 Hili ndilo pendo, kwamba tuenende sawa-
sawa na amri zake. Hii ndiyo amri yake
kama vile mlivyosikia tangu mwanzo, kwamba
mwenende katika upendo.
7 Wadanganyifu wengi, wasiokubali kwamba
Yesu Kristo amekuja katika mwili, wametokea
ulimwenguni. Mtu wa namna hiyo ni mdangany-
ifu na mpinga Kristo.

8 Jihadharini msije mkapoteza kile mlichokitenda, bali mpate kupewa thawabu kamilifu.
9 Mtu yeyote asiyedumu katika mafundisho
ya Kristo, bali akayaacha, yeye hana Mungu.
Yeyote anayedumu katika mafundisho ana Baba
na Mwana pia.
10 Msimpokee mtu yeyote anayewajia
ambaye hawaletei mafundisho haya, wala
msimkaribishe nyumbani mwenu.
11 Yeyote amkaribishaye mtu wa namna hiyo
anashiriki katika matendo maovu ya mtu huyo.

Salamu Za Mwisho

12 Ninayo mengi ya kuwaandikia, lakini sitaki
kutumia karatasi na wino. Badala yake, nataraji
kuja kwenu na kuongea nanyi ana kwa ana, ili
furaha yetu ipate kuwa timilifu.
13 Watoto wa dada yako mteule wanakusalimu.
Amen.

Biblica® Toleo Wazi Neno: Bibilia Takatifu™
Swahili: Biblica® Toleo Wazi Neno: Bibilia Takatifu™ (Bible)

copyright © 2018 Biblica, Inc.

Language: Kiswahili

Translation by: Biblica, Inc.

This translation is made available to you under the terms of the Creative Commons Attribution Share-Alike license 4.0.
You have permission to share and redistribute this Bible translation in any format and to make reasonable revisions and adaptations of this translation, provided that:

You include the above copyright and source information.

If you make any changes to the text, you must indicate that you did so in a way that makes it clear that the original licensor is not necessarily endorsing your changes.

If you redistribute this text, you must distribute your contributions under the same license as the original.

Pictures included with Scriptures and other documents on this site are licensed just for use with those Scriptures and documents. For other uses, please contact the respective copyright owners.
Note that in addition to the rules above, revising and adapting God's Word involves a great responsibility to be true to God's Word. See Revelation 22:18-19.

2021-04-12

PDF generated using Haiola and XeLaTeX on 1 Oct 2024 from source files dated 31 Aug 2023
9cbb05be-39f3-5d18-8b2a-4ba788541462